**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**TUME YA UTUMISHI SERIKALINI**

**Kumb.Na.BA.1/25/02/79** **16 Oktoba, 2024**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Tume ya Utumishi Serikalini inatangaza nafasi ya kazi ya **Afisa Takwimu Daraja la II ZPSG - 06 (Nafasi 1 – Unguja)** kwa ajili ya Taasisi ya Elimu Zanzibar:-

## ***Sifa za Muombaji:***

1. Awe Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka arobaini na sita 46.
2. Awe amehitimu Shahada ya Kwanza katika fani ya Takwimu kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
3. Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta kwa ajili ya mifumo mbali mbali ya ukusanyaji takwimu.

## ***Majukumu:***

1) Kuendeleza mfumo ya kitaifa kukusanya na kuratibu takwimu.

2) Kukusanya Takwimu pamoja na kuchukua takwimu za mifano/vielelezo "sampling"

3) Kukusanya, kusaidia kuchambua na kuwasilisha takwimu kwa wakuu wake

4) Kusaidia kutengeneza muundo(program) ya kuingiza taarifa za Takwimu katika kompyuta.

5) Kukusanya, kuchambua, kutafsiri takwimu za Taasisi, skuli na vyuo vya ualimu kwa mipango ya maendeleo.

6) Kukusanya idadi ya wafanyakazi wa Taasisi, walimu na vifaa vya ofisini na vya kufundishia.

7)Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atavyopangiwa na mkuu wake

## ***Jinsi ya Kuomba:***

- Maombi yote yawasilishwe kwa njia ya Kielektroniki kwenye mfumo wa Maombi ya Ajira (ZanAjira) kupitia anuani ifuatayo: **https://portal.zanajira.go.tz** kuanzia tarehe **16 Oktoba, 2024** hadi tarehe **30 Oktoba, 2024**.
- Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Tume ya Utumishi Serikalini **www.zanajira.go.tz**.
- Barua za maombi zitumwe kwa anuani ifuatayo kupitia mfumo wa ZanAjira (kwa njia ya kielektroniki pekee):-

  **KATIBU,**<br>**TUME YA UTUMISHI SERIKALINI,**<br>**S.L.P 1587,**<br>**ZANZIBAR**
- Muombaji anatakiwa kuainisha nafasi ya kazi anayoiomba.
- Muombaji atakaewasilisha "Progressive Report" au "Statement of Results" pekee maombi yake hayatazingatiwa.
- Kwa msaada wa kitaalamu wasiliana na Tume ya Utumishi Serikalini kupitia simu Nam. 0773101012.

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:**<br>**KATIBU,**<br>**TUME YA UTUMISHI SERIKALINI.**